



Unyanyasaji wa Kimapenzi

Nchini Australia, ni kinyume cha sheria kumnyanyasa mtu yeyote kipamenzi.

Mtu anayetokeleza unyanyasaji wa kimapenzi anaweza kwenda jela, awe mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

Australian Government (Serikali ya Australia) haivumilii unyanyasaji wa kimapenzi katika hali yoyote ile.

Unyanyasaji wa kimapenzi unafanywa kwa mtu mwingine bila ruhusa yake. Unyanyasaji wa kimapenzi kwa mwenzi, mpenzi au mwanafamilia ni kinyume cha sheria.

Unyanyasaji wa kimapenzi unaweza kujumuisha:

- kulazimisha mtu yeyote kufanya ngono au kufanya vitendo vya ngono;
- kulazimisha mtu yeyote kuangalia picha za ngono; au
- kufanya ngono au kufanya vitendo vya ngono na mtoto.

Wanawake wana haki sawa na wanaume.

Sheria za Australia zinachukulia wanawake na wanaume kuwa sawa.

Kila mtu ana haki ya kuwa katika mahusiano salama na jamii, marafiki na wapendwa wake. Unyanyasaji si sawa hata kidogo. Hakuna yeyote anapaswa kukubali kuumizwa.

Kuna huduma za kijamii nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

1800RESPECT ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **www.1800RESPECT.org.au**.

Je unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.